# KUJIANDAA KWA CHEKECHEA

Ready for K Alliance
readyforkalliance.com

CREATED BY ncfl National Center for Families Learning
familieslearning.org

## Kalinda ya Kushirikisha Familia

Karibu! Je, wajua kwamba mtoto wako yuko tayari kujifunza popote na wakati wowote? Kweli! Hata kabla hajaanza shule, mtoto wko anajifunza kila siku. Wakati wowote familia yako inazungumza au kucheza pamoja, unamsaidia mtoto wako kukua. Wewe ndiwe mwalimu wa kwanza na muhimu zaidi kwa mtoto wako!

Kuna mapendekezo kwenye kalenda hii kuhusu njia za kumsaidia mtoto wako kujifunza katika mwaka huu. Tumia shughuli zilizojumuishwa kwa njia zaidi ambazo unaweza kucheza na kujifunza nyumbani. Kalenda hii inatumia rangi kukusaidia kujua ni shughuli zipi ambazo huenda zikawa rahisi kwa watoto wa **umri wa miaka 3 hadi 5**. Baadhi ya shughuli huenda zikawa ngumu zaidi kwa watoto wa umri mdogo na zikawa bora zaidi katika mwaka **kabla ya chekechea**. Aidha, inatumiwa kubainisha **mchakato wa mpito kwa chekechea**.

Hivi punde mtoto wako atajiunga na chekechea. Huu ni wakati wa kusisimua! Familia yako huenda ikawa na maswali kuhusu kujisajili au kujiandaa kwa chekechea. Kalenda hii itawasaidia. Iko na taarifa kuhusu jinsi ya kumsajili mtoto wako shuleni. Lengo ni kwa Shule za Umma za Kaunti ya Jefferson (JCPS). Ingawa hivyo, ikiwa unateua chaguzi nyingine za shule kwa mtoto wako, huenda mchakato ukawa sawa.

Huenda umewasikia watu wakizungumza kuhusu "Utayari kwa Chekechea." Baadhi ya familia huhofu kwamba watoto wao hawako tayari na hawataweza kuhudhuria chekechea.



Hiyo si kweli! Watoto hujifunza na kukua kwa kasi yao wenyewe. Wafanyakazi shuleni watapata kumjua mtoto wako. Watafahamu kile wanachojua na kile ambacho wako tayari kufanya, Shule zitawapata watoto katika hatua walipo na kuwasaidia kufaulu.

**Iwapo familia yako inachagua Shule za Umma za Kaunti ya Jefferson (JCPS) na iko na swali, wasiliana na kituo cha mawasiliano cha JCPS kupitia 502-313-HELP (4357). Wahudumu watakuunganisha na idara ya JCPS inayofaa au mfanyakazi. Unaweza pia kutuma barua pepe kwa** jcps.help@jefferson.kyschools.us.

Mwisho, ikiwa familia yako ingependa kupata chaguzi zaidi za chekechea, nyenzo hii ina taarifa kuhusu mipango mingine ya chekechea katika jumuiya.

# SHUGHULI ZA KUSAIDIA MPITO WAKATI WOWOTE


## Miaka 3 hadi 5

- Zingatia kujisajili katika kitovu cha Metro United Way Hojaji ya Umri na Hatua. Unaweza kujisajili katika mpango huu wa uchunguzi bila malipo wakati wowote baina ya kuzaliwa na kuingia chekechea ili kujifunza zaidi kuhusu uwezo wa mtoto wako na kujifunza zaidi kuhusu shughuli ambazo zitasaidia mtoto wako kujifunza.
- Ongea na mtoto wako. Mazungumzo ya kujibizana ni muhimu katika kukuza akili ya mtoto wako. Kuzungumza na mtoto wako katika lugha yoyote husaidia akili yake kufanya miunganisho muhimu Tumia lugha ambayo ni rahisi zaidi kwako na kwa mtoto wako ukiwa nyumbani. Shughuli za Familia za Kuzungumza katika Sentensi za Maneno Tano hadi Sita.
- Kariri mashairi ya chekechea au uimbe nyimbo na watoto wako: Shughuli za Familia za Kuimba Nyimbo Sahili.
- Angalieni vitabu kwa pamoja. Sio lazima usome maneno ili uwe unasoma na mtoto wako. Zungumza naye kuhusu kile anachoona katika vitabu. Uliza maswali kama vile "Wanafanya nini?" au "Wako wapi?" Mpe mtoto wako nafasi ya kuuliza maswali pia.
- Hakikisha kuna vitabu nyumbani kwako. Nyenzo hizi zinaweza kukusaidia kusoma na mtoto wako na kufikia vitabu.
    - Maktaba ya Umma ya Bila Malipo ya Louisville inadhamini Shindano la Vitabu 1000 kabla ya Chekechea.
    - Familia zenye watoto wa umri wa miaka 0 hadi 5 katika maeneo yanayostahiki zinaweza kujisajili kwa Maktaba ya Ubunifu ya Louisville.
    - Isitoshe,familia zote zinaweza kufikia Maktaba ya Kidijitali kwa Wasomaji Wanaokua ikiwemo vitabu maalum vya Louisville.

# SHUGHULI ZA KUSAIDIA MPITO WAKATI WOWOTE

## Mchakato wa Mpito kwa Chekechea

- Hakikisha unajua wakati mtoto wako atakuwa na umri wa kutosha kuanza masomo ya chekechea. Katika Kentucky, watoto lazima watimize umri wa miaka mitano kufikia tarehe 1 Agosti ili wasajiliwa katika mwaka huo wa kiakademia. Iwapo watoto watatimu miaka 5 baina ya tarehe 2 AGosti na tarehe 1 Oktoba, familia zinaweza kuomba usajili wa mapema katika chekechea na uchunguzi baina ya tarehe 1 Desemba na tarehe 1 Machi. Watoto lazima waanza masomo ya chekechea kufikia wakati wanapotimu miaka sita.
- Iwapo familia yako inazungumza lugha nyingine kando na Kiingereza, unaweza kuomba ukalimani wakati unajadiliana na wafanyakazi wa JCPS. Wilaya ya shele inahitajika kuziwezesha familia kufikia mkalimani ili kusaidia mawasiliano na wafanyakazi wa shule. JCPS imeunda Kadi za Nazungumza ili kusaidia familia katika kuomba ukalimani.
- Iwapo una shauku kuhusu maendeleo ya mtoto wako, wasiliana na daktari wako. Kuna mipango katika jumuiya yako kama vile Hatua za kwanza (First Steps) au Elimu ya mapema ya JCPS ambayo inaweza kusaidia. Isitoshe, unaweza kuwasiliana na Huduma za JCPS za Elimu kwa Watoto wenye Uwezo wa Kipekee (ECE) iwapo unaamini mtoto wako anahitaji usaidizi wa ziada katika chekechea.
- Talii nyenzo za JCPS Ready4K resources. Nyenzo nyingine ni JCPS Checklist ambayo familizi zinaweza kukagua ili kuelewa jinsi watoto wako tayari kukua na kujifunza katika chekechea.



Ready for K Alliance
readyforkalliance.com

CREATED BY ncfl National Center for Families Learning
familieslearning.org







Kalenda hii itakuongoza katika mchakato wa kuchagua shule na kumsajili mtoto wako katika chekechea. Aidha, iko na shughuli za kumsaidia mtoto wako kukua na kujifunza!

Ready for K Alliance
readyforkalliance.com

CREATED BY ncfl
National Center for Families Learning
familieslearning.org

# SEPTEMBA

## MIEZI 11 ILI KUJIUNGA NA CHEKECHEA

### Miaka 3 hadi 5

- Ratiba ni muhimu! Unda ratiba kuhusu chakula, saa ya kuoga, au saa ya kulala. Itamsaidia mtoto wako kuhisi salama na kujisimamia wakati anajua kile kinachofuata: Kanuni Sahili na Mazoea katika Shughuli za Familia.

### Mchakato wa Mpito kwa Chekechea

- Anza kutalii chaguzi za familia yako za chekechea. Unaweza kuanzia kwenye Tovuti ya kutafuta shule ya JCPS. JCPS pia inatoa Miongozo ya Kuchagua Shule katika Kihispania, Kiarabu, Kiswahili, Kinepali, and Kisomali. Familia pia zinaweza kuzuru tovuti za shule na kuzungumza na marafiki na wafanyakazi wenza.
- Je, ni shule ya aina gani itaafiki zaidi mtoto wako na familia yako? Mwongozo wa Kuchagua Shule za Msingi unaeleza makundi ya shule, shule za kuvutia, na mipango ya kuvutia katika JCPS. Tafuta shule bora zaidi kwa mtoto wako. Familia yako pia huenda ikatalii chaguzi nyingine za chekechea katika jumuiya yetu.
- Kuwa makini kwa matukio ya kipkee katika jumuiya! Ofisi ya Kuchagua Shule ya JCPS ina wafanyakazi katika matukio ili kusaidia familia kuchagua shule, usajili na maombi. (Usajili ni kufungua akaunti ya JCPS mtandaoni na kuonyesha ithibati za anwani. Maombi ni kuomba chaguzi zako za shule.)



# OKTOBA

## MIEZI 10 ILI KUJIUNGA NA CHEKECHEA

### Miaka 3 hadi 5

- Hesabu na uzungumze na mtoto wako kuhusu nambari. Unaweza kutumia vidole vyako kuhesabu. Mfanyishe mtoto wako mazoezi ya kuhesabu vitu wakati mnatembea au kwenda dukani. Shughuli za Familia za kuhesabu kwa mfuatano hadi 30.

### Mchakato wa Mpito kwa Chekechea

- Hudhuria Maonyesho ya shule ya JCPS. Unaweza kuzungumza na wafanyakazi kutoka kila shule ya msingi na kujifunza zaidi kuhusu chaguzi za shule zinazopatikana kwa familia yako. Unaweza pia kujifunza kuhusu michakato ya usajili na maombi kwa JCPS. Wakalimani watakuwepo kuisaidia familia yako kuwasiliana katika lugha mnayopendelea.
- Iwapo familia yako inachagua JCPS, msajili mtoto wako kwa chekechea mtandaoni. Hata kama una watoto wengine wanaohudhuria JCPS, sharti umsajili mtoto wako wa umri wa miaka 5 kwa chekechea. Usajili huhitaji hatua mbili:
    - Kujaza fomu mtandaoni. Unahitaji jina lako na la mtoto wako, tarehe ya kuzaliwa, jinsia, nambari ya simu, na anwani ya barua pepe.
    - Wasilisha ithibati ya anwani: Kama vile bili ya maji, karatasi ya malipo kazini, hati ya kukodi nyumba iliyotiwa sahihi, au mawasiliano baina yako na asasi ya serikali. Iwapo familia yako haina anwani ya kudumu, unaweza kuwasiliana na Ofisi ya Ufikiaji na Fursa kupitia 502-485-3650. Huenda wakaweza kukusaidia.
- Iwapo utahitaji usaidizi, unaweza kuratibu miadi ya usajili na JCPS. Aidha unaweza kuomba mkalimani. Kumbuka, usajili ni kufungua akaunti ya JCPS mtandaoni na kuonyesha ithibati za anwani.



# NOVEMBA

## MIEZI 9 ILI KUJIUNGA NA CHEKECHEA

### Mwaka kabla ya kujiunga na Chekechea

- Zungumza na mtoto wako kuhusu maneno na herufi ambazo wanaona katika mazingira yao. Anza kwa herufi katika jina la mtoto wako. Kisha uzidi kuongeza herufi mpya kidogo kidogo. Kuzungumza kuhusu herufi na maneno huwasaidia watoto kujifunza kwamba ishara hizi hubeba ujumbe: Shughuli ya Familia Kutumia Michoro ovyo na Uchoraji Kueleza Mawazo.

### Mchakato wa Mpito kwa Chekechea

- Shule nyingi huwa na siku ya maonyesho au hutoa fursa za kuzuru. Unaweza kuiona shule na kukutana na wafanyakazi. Hii ni njia bora ya kujifunza zaidi kuhusu chaguzi zako za shule. Piga simu shuleni uulize kuhusu maonyesho na fursa za kuzuru. JCPS iko na orodha ya matukio kwa familia ambazo zina ilhamu na shule zake. Familia zinaweza kuomba ukalimani katika hafla za JCPS.
- Iwapo unachagua JCPS, familia yako inaweza kutuma maombi Novemba. Kutuma maombi ni wakati unapoteua chaguzi zako za kwanza kwa mtoto wako. Hakikisha unafanya hivi kufikia Desemba, ili mtoto wako apate nafasi nzuri ya kuhudhuria shule ambazo zimwafiki zaidi.



# DESEMBA

## MIEZI 8 ILI KUJIUNG NA CHEKECHEA

### Miaka 3 hadi 5

- Mtoto wako anaweza kuandika jina lake kwenye kadi au vibandiko vya zawadi. Msaidie kufanya mazoezi ya kunadika jina lake. Unaweza kumwonyesha mtoto wako jinsi ya kushika penseli au kalamu wakati wa kuandika. Shughuli ya Familia za Kusoma na Kuandika Jina Lake.
- Mpe mtoto wako nafasi ya kuchora! Anaweza kuunda sanaa. Michoro yake huenda ikaonekana kuwa ovyo, lakini ina maana kwa mtoto wako. Muulize mtoto wako akueleze kuhusu michoro yake: Shughuli ya Familia Kutumia Picha Kueleza Kisa.

### Mchakato wa Mpito kwa Chekechea

- Makataa ya kutuma maombi kwa JCPS ni Desemba. Hakikisha kwamba familia yako imeomba shule ambazo zinaafiki zaidi mahitaji ya mtoto wako!



# JANUARI

## MIEZI 7 ILI KUJIUNGA NA CHEKECHEA

NEW YEAR

**Miaka 3 hadi 5**

- Msimu wa baridi kali unamaanisha makoti na Kofia! Msaidie mtoto wako kujifunza jinsi ya kujivisha nguo. Huenda ikachukua muda mrefu, lakini inawatia moyo kuweza kujisimamia zaidi. Kujua jinsi ya kufunga vifungo, zipu, na jinsi ya kuvaa mavazi ni stadi muhimu za maisha: Shughuli ya Familia Kufunga na Kufungua Nguo zake Mwenyewe.
- Zungumza na mtoto wako kuhusu rangi na maumbo. Unaweza kupata rangi na maumbo mahali mnaishi, dukani, au mkiwa katika matembezi nje. Jaribu kupanga mchezo wa "Nimeona" (I Spy) na mtoto wako: Nimeona kwa jicho langu ndogo kitu ambacho ni . Unaweza pia kumuomba mtoto wako atafute vitu vitatu ambavyo ni vya rangi sawa: Shughuli ya Familia Kutambua, Kutaja na Kurudufu Maumbo ya Kimsingi.



# FEBRUARI

## MIEZI 6 ILI KUJIUNGA NA CHEKECHEA

### Miaka 3 hadi 5

- Tumia maneno yanayoashiria hisia kama vile furaha, huzuni, kukasirika, kuogopa, na kusisimka kwa mtoto wako. Watoto wanahitaji maneno ya kuzungumzia hisia zao. Aidha, unaweza kutumia maneno yanayoashiria hisia zako wakati uko na mtoto wako. Huenda ukawa umesisimka kwenda mahali au ukawa na huzuni inaponyesha: Shughuli ya Familia ya Kueleza Mahitaji yake Mwenyewe.
- Tembelea maktaba na mtoto wako. Ni njia nzuri ya kujifunza katika msimu wa baridi. Masimulizi na shughuli nyingine za maktabani ni mahali pazuri sana pa kukutana na kuzungumza na watoto na familia zingine pia! Familia zote zinaweza kufurahia mipango ya maktaba. Familia yako huenda ikaweza kupata kadi ya mkataba kupitia Maktaba ya Umma ya Bila Malipo ya Louisville.
- Zungumza na mtoto wako kuhusu sauti. Sikiliza kila kitu: muziki, sauti za ndege au wadudu, kupiga makofi na hata kicheko. Msaidie mtoto wako kusikiliza na kuzungumza kuhusu jinsi sauti zinafanana na kutofautiana.



# MACHI

## MIEZI 5 ILI KUJIUNGA NA CHEKECHEA

### Miaka 3 hadi 5

- Nenda nje ukaruke na kucheza na mtoto wako. Ziara za bustani ya michezo zinafurahisha na mtoto wako anaweza kupanda daraja na kucheza bembea. Shughuli hizi husaidia kujenga misuli huku zikiimarisha mwambatano na uwezo wa kusimama bila kuyumba: Shughuli ya Familia Kukimbia, Kuruka, na Kupanda juu.

### Mchakato wa Mpito kwa Chekechea

- Watoto wanahitaji kupokea chanjo na uchunguzi wa mwili, uchunguzi wa meno, na macho wanapoanza masomo ya chekechea. Msimu wa kuchipua ni wakati bora wa kufanya miadi na daktari na, daktari wa meno. Unaweza kuzuru Vituo vya Afya ya Familia upate watoa huduma, huduma, na taarifa katika lugha unayopendelea.
- Iwapo familia yako inazungumza lugha ya ziada nyumbani, huenda mtoto wako akaweza kupokea huduma za Mwanafunzi wa Kiingereza kutoka kwa JCPS. Unaweza kuomba uchunguzi kufikia miezi sita kalba ya kuanza chekechea. Wasiliana na idara ya Kiingereza kama Lugha ya Pili (ESL) upate usaidizi.



# APRILI

## MIEZI 4 ILI KUJIUNGA NA CHEKECHEA

### Miaka 3 hadi 5

- Mhimize mtoto wako aweze kujilisha. Mruhusu afanye mazoezi ya kutumia uma au kijiko. Familia pia zinaweza kuwafunza watoto wao kufungua vifurushi. Kazi hii ya mikono itasaidia kuipa mikono ya mtoto wako nguvu, ili aweze kujifanyia mambo mengi kwa kujisimamia. Shughuli ya Familia Kujilisha kwa Kutumia Vyombo.

### Mchakato wa Mpito kwa Chekechea

- Watoto wanahitaji kupokea chanjo na uchunguzi wa mwili, uchunguzi wa meno, na macho wanapoanza masomo ya chekechea. Msimu wa kuchipua ni wakati bora wa kufanya miadi na daktari na, daktari wa meno. Unaweza kuzuru Vituo vya Afya ya Familia upate watoa huduma, huduma, na taarifa katika lugha unayopendelea.
- Iwapo familia yako inazungumza lugha ya ziada nyumbani, huenda mtoto wako akaweza kupokea huduma za Mwanafunzi wa Kiingereza kutoka kwa JCPS. Unaweza kuomba uchunguzi kufikia miezi sita kalba ya kuanza chekechea. Wasiliana na idara ya Kiingereza kama Lugha ya Pili (ESL) upate usaidizi.



# MEI

## MIEZI 3 ILI KUJIUNGA NA CHEKECHEA

### Mwaka kabla ya kujiunga na Chekechea

- Fanya mazoezi ya kujibu maswali kama vile, "Unaishi wapi?" na "Nambari yako ya simu ni gani?" Mtoto wako anahitaji kujua taarifa hii iwapo kuna dharura: Shughuli ya Familia Kujua Taarifa ya Kibinafsi.
- Pitia vitabu kuhusu shule. Unaweza kuzungumza kuhusu jinsi wahusika wanaunda urafiki na kujifunza shuleni: Shughuli ya Familia Kucheza na Kushiriki na Watoto Wengine.

### Mchakato wa Mpito kwa Chekechea

- Angalia iwapo mtoto wako anastahiki Mpango wa JCPS Camp Ready 4K - Mpango wa kuwakaribisha watoto katika chekechea. Usajili aghalabu hufanyika mwanzoni mwa Mei. Mpango huu hujaa haraka, kwa hivyo jisajili mapema!
- Kuwa makini kwa taarifa kutoka shule yako kuhusu matukio ya makaribisho msimu wa joto na mwanzoni mwa msimu wa vuli. Shule nyingi zitatuma barua au barua pepe kwa familia yako.



# MSIMU WA JOTO

## MIEZI 2 ILI KUJIUNGA NA CHEKECHEA

### Miaka 3 hadi 5

- Mashirika mengi ya kijamii hutoa mipango ya msimu wa joto kwa familia. Jiandikishe kwa Mpango wa Kusoma katika Msimu wa Joto au katika mpango wa Louisville Cultural Pass.

### Mchakato wa Mpito kwa Chekechea

- Mtoto wako atahitaji nyenzo za kurejea shuleni kama vile mkoba na mavazi. Baini kile ambacho mtoto wako anahitaji katika shule yake. Angalia orodha kwenye tovuti ya shule. Fanya mpango wa kuweka tayari vitu vingi katika orodha hiyo kadri iwezekanavyo. Washiriki wengi wa jumuiya hutoa zawadi za nyenzo zinazohitajika.
- Iwapo familia yako itahitaji usaidizi, wasiliana na Mratibu wa Kituo cha Kusaidia Familia (FRC) katika shule yako. Kituo cha kusaidia familia kinaweza kuisaidia familia yako kufikia Mpango wa JCPS wa Msaada wa Mavazi (CAP) ambao unaweza kutoa sare na mavazi mengine bila malipo. Aidha wanaweza kusaidia na nyenzo nyingine na miadi ya uchunguzi wa afya.
- Ikiwezekana, tembea, endesha baiskeli au gari karibu na shule ya mtoto wako katika msimu huu wa joto. Mwonyeshe mtoto wako jengo na uzungumze naye kuhusu ni jinsi atajifunza mambo mengi shuleni. Hii itamsaidia mtoto wako kujua kwamba shule ni mahali salama ambapo ujifunzaji unafanyika.



# AGOSTI

## TUNAINGIA CHEKECHEA!

### Mwaka kabla ya kujiunga na Chekechea

- Wiki mbili kabla ya shule kuanza, zungumza na mtoto wako kuhusu siku yake ya kwanza shuleni. Msaidie kupanga shughuli za mazoea kama vile kupanga nguo za kuvaa usiku wa kuamkia shule na kupanga mkoba wao: Shughuli ya Familia Kufuatilia Vitu vya Kibinafsi.
- Jadili jinsi mtoto wako atafika shuleni. Je, atatembea? Kusafiri kwa basi? Au ataendeshwa na rafiki au jamaa? Tazama Shughuli ya Familia Kujitenga kwa Urahisi Kutoka kwa Wazazi na Familia.

### Mchakato wa Mpito kwa Chekechea

- Jaribu kuhudhuria hafla kama vile mkutano wa chekechea, mkutano usio rasmi, na mkutano na mwalimu ambao utaruhusu familia yako kutembelea shule. Kadri mtoto wako anavyofahamiana na shule yake, atahisi kuwa slama na kufurahia zaidi kuanza masomo ya chekechea.
- Familia yako huenda ikastahiki kupokea chakula bila malipo au kupunguziwa gharama ya chakula shuleni Baini iwapo shule yako inatoa chakula bila malipo kwa wanafunzi wote au iwapo unahitaji kujaza fomu. Iwapo una maswali, wafanyakazi wa ofisi ya mtoto wako wataweza kukusaidia.



Ready for K Alliance
readyforkalliance.com
CREATED BY ncfl National Center for Families Learning
familieslearning.org

# SEPTEMBA

## TUNAINGIA CHEKECHEA!

### Mwaka kabla ya kujiunga na Chekechea

- Mwezi wa kwanza katika chekechea huenda ukawa wenye furaha na wa kusisimua. Mfurahie mtoto wako anapofanya na kujifunza mambo mapya. Usiwe na wasiwasi ikiwa mtoto wako atachukua wiki chache kuzoea kuamka, kujiandaa kwa ajili ya shule na kwenda shuleni. Unaweza kumsaidia kwa kuwa na ratiba, kupata usingizi wa kutosha, na kutumia muda pamoja mkisoma au kucheza.
- Kuanza shule ni tofauti kwa kila mtoto Mtoto wako huenda akapenda shule kutoka mwanzo au akachukua muda kuzoea ratiba mpya. Jambo mojawapo muhimu zaidi ambalo mnaweza kufanya kama familia ni kuunganika na mwalimu wa mtoto wako mapema na mara kwa mara. Jifunze njia bora ya kuzungumza na mwalimu wa mtoto wako kuhusu maswali ambayo huenda uko nayo au taarifa ambayo unataka kushiriki kuhusu mtoto wako.

